# Namna ya Kuimarisha Utamaduni wa Kusimulia Hadithi katika Jamii ya Wamasaaba nchini Uganda

Wanyenya Willy, Rocha Chimerah & Nancy Jumwa Ngowa


## Ikisiri
Kwa muda mrefu Wamasaaba wamekuwa wakishughulika na usimulizi wa hadithi kikamilifu katika jamii yao lakini siku hizi hawashughuliki tena na jambo hilo. Wengi wao hasa wale ambao ni wasomi hawaoni umuhimu wa kusimulia hadithi kwani huchukulia jambo hili kuwa la watu ambao hawajaelimika. Hivyo utafiti wetu umefanywa ili kufafanua mambo yanayorudisha nyuma usimulizi wa hadithi katika jamii yao na kupendekeza hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuimarisha usimulizi wa hadithi katika jamii hiyo. Utafiti huu unakusudia kujibu maswali mawili: ni mambo gani ambayo yamefanya Wamasaaba wa Bududa wakose kuendeleza utamaduni wao wa kusimulia hadithi? Ni nini ambacho kinaweza kufanywa ili Wamasaaba waendeleze usimulizi wa hadithi katika jamii yao? Mtafiti alikumbuka miaka ya 1960 na 1970 ambapo wazazi walisimulia watoto wao hadithi akaona kwamba kuna mambo mengi sana ambayo watoto wa sasa wanayakosa. Alikumbuka jinsi alivyosimuliwa hadithi na babake alipokuwa mtoto. Mara kadhaa, mtafiti alimtembelea bibi mzaa mama ambaye pia alikuwa na kipawa cha kusimulia hadithi. Katika miaka ya 1970 kwenye shule za msingi, usimulizi wa hadithi pia uliratibiwa. Wakati huo watoto waliitwa mbele ya darasa mmoja baada ya mwingine na kusimulia hadithi katika lugha ya mama, yaani LuMasaaba. Wale walioshindwa waliadhibiwa. Haya ni mambo ambayo hayapo tena sasa ikilinganishwa na miaka ambayo imetajwa.


## 1.0 Utangulizi
Makala hii inachunguza masimulizi ya kinathari katika jamii ya Wamasaaba na kudhihirisha hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kufufua na kuimarisha utamaduni wa kusimulia hadithi miongoni mwa Wamasaaba. Utafiti huu umefanywa ili kudhihirisha kuwa hadithi ni utanzu muhimu wa fasihi simulizi katika jamii za Kiafrika, hususani Wamasaaba wa Bududa nchini Uganda. Hivyo, utafiti huu umelenga kuwahimiza vijana, shule, vyuo, wafanyakazi katika vituo vya redio na Wamasaaba kwa ujumla waimarishe utamaduni huu. Tumeigawa makala yetu katika sehemu kuu saba: sehemu hizo ni utangulizi ambao unatambulisha mada husika ya makala; usuli wa jamii ya Wamasaaba, utamaduni na imani zao; uhusiano wa mila (kama vile kufanya tohara kwa vijana wa kiume) na fashihi simulizi (hadithi katika kipera cha visasili); nadharia iliyotumika, mapitio ya maandishi, na uchambuzi wa matokeo ya utafiti. Mwisho kabisa ni hitimisho.

Mahojiano, hojaji na uchunguzi shiriki ndizo mbinu za ukusanyanji wa data zilizotumika katika utafiti huu. Mtafiti alitumia mahojiano kwa sababu yalimwezesha kupata taarifa za kiasili, sahihi na kwa ufafanuzi zaidi, jambo ambalo hojaji isengelitekeleza. Ni kwa kupitia mahojiano pia tuliweza kurekodi hadithi mbalimbali ambazo zilisimuliwa na watafitiwa. Mbinu ya pili ni hojaji. Hojaji zilihusu dhima, maudhui, hali ya masimulizi ya kihadithi na hatua za kuboresha utendaji wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba. Mahojiano na hojaji zetu ziliwalenga wakulima na wanafunzi ambao walikuwa wakiishi nyumbani na wazazi wao. Kwa upande wa uchunguzi shiriki, mtafiti alichunguza na kushiriki utendaji wa masimulizi ya kinathari katika jamii husika. Utafiti huu ulihusisha

watu 120 kutoka mitaa minne ya kata ya Bukigai wilayani Bududa; wahojiwa 30 katika kila mtaa (wanaume 10, wanawake 10 na vijana 10). Wahojiwa waliteuliwa kutoka rika tofauti (miaka 18 hadi 70) na jinsi zote mbili, hii ni kwa sababu wengi wao wanaweza kujieleza bila matatizo, wanajua tamaduni zao vizuri, wamepata kushuhudia matukio kadhaa wa kadhaa katika jamii yao kama vile vita vya kikabila, majanga ya njaa, ndoa za kiutamaduni, ibada za kijadi na kadhalika. Katika makala hii, mtafiti ametumia Nadharia ya Ethnografia na Utendaji.

## 2.0 Wamasaaba: Jiografia, Shughuli za Kiuchumi, Imani na Mila zao

Kulingana na maelezo ya wakazi wa Bududa, neno Wamasaaba humaanisha watu wa ukoo wa Masaaba. Watu hawa wanaamini kwamba Masaaba ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa jamii yao na wao wenyewe wanajiita Bamasaba. Katika lugha ya Kiswahili nimewaita Wamasaaba badala ya Bamasaba kwa sababu katika lugha ya Kiswahili huwa tunatumia kiambishi awali ’wa’ tunapotaja watu katika hali ya wingi. Kwa mfano, Wagiriama, Waswahili, Waluo, na kadhalika. Wao wanapatikana katika Mlima Elgon ambao ni mojawapo ya milima mirefu sana barani Afrika. Mlima huu unapatikana kwenye mpaka baina ya nchi ya Uganda na Jamhuri ya Kenya. Kwa hiyo, katika utafiti huu mtafiti anachunguza sababu ambazo zimepelekea masimulizi ya kinathari kutoweka katika jamii hiyo na kubainisha hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuimarisha utamaduni wa kusimulia hadithi.

Kulingana na ramani ya Uganda inayoonesha mipaka ya wilaya mbalimbali ambayo iliandaliwa na Wizara ya Serikali za Mitaa, wilaya ya Bududa inapatikana mashariki mwa Uganda kwenye mpaka na nchi ya Kenya. Wilaya hii inapitiwa na mto mkubwa kiasi unaoitwa Manafa. Pia, kuna vijito vidogovidogo kama vile Suume, Wolukusi, Tsutsu, Tumbu, Malabaasi na Maaba ambavyo hujiunga na Manafa katika vituo mbalimbali na hivyo kuongeza ukubwa wake. Aidha, kuwapo kwa Mlima Elgon na msitu mkubwa kileleni kumeiweka Wilaya ya Bududa katika nafasi nzuri ya kupokea mvua karibu kila mwezi. Hali hii imewawezesha wakazi wa Bududa kujimudu kiuchumi.

Utafiti huu ulifanywa katika kata ya Bukigai, tarafa ya Manjiya wilayani Bududa. Baada ya Uganda kupata uhuru mwaka 1963, kata ya Bukigai iliundwa kwa mitaa minne. Mitaa hiyo ni Bumatanda, Bunamubi, Bunakhayoti na Bushiribo. Wakati ule ambapo nchi hiyo ilipata uhuru, Kata ya Bukigai ilipakana na Kata za Bushika, Bududa, Bulucheke na Kaato ambayo inapatikana wilayani Manafwa. Baadaye, mitaa ambayo iliunda kata ya Bukigai iligawanywa na mitaa mingine ikapatikana. Kupatikana kwa mitaa mingine kulisababisha mahitaji ya Kata yenyewe pia kugawanywa. Basi, Bukigai ya mwanzo ikagawanywa na kata zingine mbili zikapatikana. Kata hizi mbili zilizopatikana ni Bushiribo na Nabweya. Kwa hivi sasa, Kata ya Bukigai imeundwa kwa mitaa kama Bumatanda, Bumakuma, Bunaporo na Bunamubi. Miongoni mwa mitaa hii, Bunaporo na Bunamubi ni mitaa ambayo imebuniwa hivi karibuni. Kwa wakati huu,

Bukigai inapakana na kata za Bushiribo, Nabweya, Bulucheke, Bubiita, Nalwanza na Kaato. Kwa hiyo, utafiti huu ulifanywa ndani ya mipaka ya Bukigai ya sasa wala siyo ya kwanza. Sababu kuu ilikuwa ni kufanya uchunguzi wa kina. Wilaya ya Bududa kwa upande wa mashariki inapakana na eneo la Mlima Elgon. Kwa hivi sasa, eneo hili limegawanywa mara tano na hivyo kuwa na Wilaya tano tofauti. Wilaya hizo ni Mbale, Sironko, Manafwa, Bududa na Bulambuli. Wilaya hizi tano zinapatikana upande wa magharibi wa Mlima Elgon ambao unapatikana mpakani mwa nchi ya Kenya.

Wamasaaba wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kulingana na mtafiti, ambaye ni mzaliwa na pia mkazi, Wamasaaba wa Bududa ni wakulima. Chakula kikuu cha watu wa Bududa ni ndizi. Mazao mengine ni mahindi, maharagwe, viazi, maboga, mihogo, matunda, nyanya, vitunguu, kabichi na kunde. Mazao haya hupandwa kwa ajili ya chakula na biashara. Hali kadhalika, vijito vinavyopatikana katika Wilaya ya Bududa vimewawezesha vijana kushughulika na kazi za uvuvi, uchimbaji wa mchanga wa kujengea, ukusanyaji wa mawe kwa ajili ya kutengeneza changarawe na kokoto. Baadhi ya wakazi huchota maji na kuwauzia wenye vilabu vya pombe ya kienyeji na wenye mikahawa. Samaki huvuliwa kwa kutumia kulabu au dawa inayotengenezwa kwa majani ya mitishamba ambayo ina uwezo wa kulevya samaki na hivyo wao hushikwa bila shida yoyote. Baadhi ya wakazi huenda msitu wa Mlima Elgon kuvuna mimea ya *kamalea* na kuiuza. Mmea huu hutumiwa kama mboga. Wakazi wengine, hususani wale wanaoishi karibu na msitu hujishughulisha na kazi ya kuwinda wanyama. Miongoni mwa wanyama wanaowindwa ni ndovu, nguruwe mwitu, swala na kadhalika.

Wakazi wa Bududa pia hufuga wanyama kama vile ng’ombe, nguruwe, mbuzi, mbwa, paka, kondoo na sungura. Wao wanapendelea sana kufuga mafahali ambao huwa wakiwapiganisha siku ya Jumamosi wanapopelekwa bondeni kunywa maji yenye chumvi. Kwa kawaida ng’ombe hupenda kulamba chumvi. Kwa hiyo, badala ya kuwanunulia chumvi huwa wanapelekwa bondeni kunywa maji yenye chumvi ya bure. Mwenye fahari anayeshinda katika kupigana huko hujisifu kwa kazi nzuri aliyoifanya, yaani ya kulisha fahali wake vizuri. Wanyama hao huuzwa na hivyo huwaletea wafugaji pesa ambazo zinawawezesha kugharamia mambo mbalimbali. Vilevile wakazi wa Bududa ni maarufu kwa kutengeneza pombe za kienyeji kama vile *busela*, *inguli* na *indali ye kamatole*. Aina hizi tatu za pombe huuzwa na hivyo huongezea mapato ya wakazi wa Bududa.

Kwa mjibu wa Nzita na Mbaga (1998), Wamasaaba wa Bududa na wale wanaoishi katika maeneo mengine ya Bugisu kwa jumla huamini kwamba mtu huendelea kuwapo hata baada ya kufariki. Wao wanaamini kuwa roho za jamaa waliokufa huwa zikirejea nyumbani na zina nguvu za kuathiri jamaa wa karibu. Kwa hiyo, kama ilivyo kawaida, mtoto mchanga akililialia usiku, Wamasaaba huamini kwamba mtoto huyo anasumbuliwa na roho za jamaa waliokufa. Hali kama hii ikitokea, wao huandaa karamu kubwa sana na

hivyo mzee mmoja huita majina ya jamaa wa karibu waliokufa waje washiriki ili waridhike na hivyo waache kumsumbua mtoto huyo. Vilevile, kwa mujibu wa Nzita na Mbaga (1998), ikiwa mtu aliyekufa aliacha mashamba, Wamasaaba huamini kwamba wakati mwingine mtu huyo hurejea na kuzuru mashambani kwa ajili ya kuyakagua na kuona jinsi yalivyo. Kwa hiyo, mara nyingi wazazi huwaonya watoto wao wasitembeetembee mashambani hasa mchana wa jua kali kwa sababu huu ni wakati unaodhaniwa kuwa roho za watu waliokufa hurejea na kurandaranda duniani. Vilevile, si rahisi Mmasaaba wa jadi kula chakula akakimaliza kabisa kwa kuhofia kuwa jamaa waliokufa watarejea halafu wakose chakula. Inaaminika kuwa wakikosa chakula huleta balaa katika familia.

Vilevile, Wamasaaba wameweka imani zao katika miungu kwa jina maarufu *Wele matsakha*. Wamasaaba huamini kwamba miungu hutawala maisha yao na isiporidhishwa inaweza kuzusha balaa. Kwa sababu hii, mabinti wengi katika jamii wakikosa kuzaa watoto, Wamasaaba husema kwamba miungu imekasirishwa na matendo yao mabaya. Vilevile, mtu akishikwa na ugonjwa wa ajabu wao hudai kwamba ugonjwa huo umetokana na kukasirika kwa miungu. Kwa hiyo, mara nyingi karamu mbalimbali huandaliwa miongoni mwa Wamasaaba kwa ajili ya kuridhisha miungu hiyo. Nzita na Mbaga (1998) wanasema kuwa wakati mwingine kuku au mbuzi huchinjiwa mtoni na makaburini au ngoma maalumu ijulikanayo kama *Shikongo* huchezwa inapogundulika kuwa mabinti wengi katika jamii hawazai watoto. Wakati mwingine, watu huwa na hofu ya kuua baadhi ya ndege mwitu au nyoka fulani kwa kudai kwamba wana uhusiano nao wa kijamii. Kuna wale ambao hawali hata nyama ya kichwa cha kondoo kwa sababu ya imani kama hizo.

Nzita na Mbaga (1998) wanaendelea kusema kuwa Wamasaaba wanaamini kuwa nguvu za watu waliokufa zinaweza kuathiri vijana wanaotaka kutahiriwa na hivyo wakose kusimama imara au hata wakimbie kabla hawajaguswa na ngariba. Jambo hili huwafanya wazazi wa vijana husika watende mambo kadhaa kwa ajili ya kuridhisha roho hizo. Mambo muhimu hapa ni kuandaa pombe na kuchinja wanyama. Hii ni kwa sababu, Wamasaaba huamini kwamba roho za watu waliokufa hufurahia kunywa pombe na kula nyama. Kwa hiyo, ni lazima kwa kila mzazi wa kijana anayetarajiwa kutahiriwa kutekeleza mambo kadhaa yanayodhamiria kuridhisha roho za watu waliokufa ili waweze kuwakinga vijana husika. Aidha, vijana hao hulishwa mitishamba na kupakwa miili yao unga wa bwimbi uliochaganywa na maji. Unga huu huchukuliwa kuwa ni kinga dhidi ya pepo wabaya wanaoweza kuathiri vibaya vijana husika. Imani hizi pia ni muhimu kwa sababu zimewekea fasihi simulizi ya Wamasaaba msingi. Hii ni kwa sababu kuna hadithi nyingi zenye maudhui yanayohusiana na imani hizo. Sehemu ifuatayo inazungumzia uhusiano wa mila (kufanya tohara kwa vijana wa kiume) na fashihi simulizi (hadithi katika kipera cha visasili).

**3.0 Uhusiano wa Mila (kufanya tohara) na fashihi simulizi (visasili)**

Miongoni mwa mila za Wamasaaba ni kufanya tohara kwa vijana wao wa kiume. Hivyo, tohara ina chimbuko lake maalumu. Kwa mujibu wa utafiti wetu kwa wakazi wa Bududa kuna hadithi na nyimbo nyingi zinazozungumzia mambo ya tohara miongoni mwa Wamasaaba. Kulingana na maelezo yao, asili ya tohara miongoni mwao imetokana na visasili kama vitatu hivi. Kisasili cha kwanza kinashikilia kwamba Mmasaaba ambaye anaaminika kuwa mwanzilishi wa jamii ya Wamasaaba alizaa wanawe wanne wa kiume. Wana hao walikuwa ni Mugisu, Mubuya, Wanale na Mungokho. Inasemekana, baadaye kila mtoto alipewa sehemu yake ya ardhi. Wanale alipewa kilima cha Wanale, Mubuya akapewa eneo la Bududa, Mugisu alipewa eneo la Budadiri halafu Mungokho akapewa Bungokho eneo ambalo tohara huzinduliwa kila mwaka wa tohara. Eneo hili la Bungokho kwa hivi sasa linajulikana na kuheshimiwa sana na Wamasaaba wote kama eneo ambako tohara ilianzia. Kisasili hiki kinaeleza kwamba siku moja, Mungokho alipokuwa akitekeleza shughuli zake za kila siku, alimkurupusha mnyama pori ambaye alikimbia kuelekea msitu wa Mlima Elgon. Inasemekana Mungokho alimkimbiza mnyama huyo hadi kule msituni na kwa bahati mbaya, hakuweza kumkamata. Wakati wa jioni alipokuwa kule msituni bila kujua la kufanya, aliona moshi ukipaa angani kwenye eneo moja. Yeye alikuwa na hamu ya kutaka kujua chanzo cha moshi huo ni nini. Kwa hiyo, aliamua aende karibu ili aweze kuthibitisha chanzo chake. Alipofika karibu aliona kwamba hapo palikuwa masikani pa mtu. Hii ni kwa kuwa yeye alikuwa amefika Iburwa katika jamii nyingine ya watu wanaojulikana kama Barwa. Mungokho aliamua kuingia kule na kubaini kwamba mzee wa hapo alikuwa na mabinti warembo sana. Inasemekana Mungokho aliomba ruhusa kwa mzee huyo ya kutaka amuoe binti mmoja.

Mungokho alipewa msichana mmoja na akarudi naye kwake kule Bungokho. Waliishi pamoja kwa muda na kujaaliwa kupata watoto. Hapo awali, watoto hao walikuwa na afya nzuri lakini baadaye hali yao ilibadilika na kudhoofika sana kwa ugonjwa. Kulingana na kisasili hiki, Mungokho alijaribu kutibu watoto wake bila mafanikio. Ilimbidi aende kushauriana na wakwe zake kuhusu dhiki iliyompata. Alipofika huko, alishauriwa arudi nyumbani akawatahiri watoto wake. Kwa hiyo, Mungokho alirudi nyumbani akafanya hivyo. Baada ya kuwatahiri watoto hao ugonjwa ambao ulikuwa ukiwasumbua ulitoweka. Basi, kuanzia hapo Mungokho akawa akiwatahiri wanawe wa kiume na kitendo hicho kikaendelea katika jamii mpaka sasa. Hii ndiyo sababu wakati wa kufungua sherehe za tohara ukiwadia, Wamasaaba wote hukusanyika kule Bungokho kwenye uwanja wa Bumutoto. Na miongoni mwa nyimbo zinazoimbwa ni ule usemao:

> *kumusambwa kwefe ee kwama iburwa ee o yaya o,*
> tafsiri: *pepo wetu wa tohara alitoka kule Iburwa.*

Kisasili cha pili kinaelezea kuwa mtu mmoja wa jamii ya Wamasaaba alitaka kumuoa msichana mmoja kutoka Iburwa. Lakini msichana huyo alisema isingewezekana yeye kuolewa na mtu ambaye hakuwa ametahiriwa. Kwa hiyo, jamaa huyo alilazimika

kutahiriwa. Na kuanzia hapo Wamasaaba wakawa wakitahiriwa mpaka sasa. Kisasili cha tatu ni kile kinachoeleza kuwa hapo kale kulikuwa na soko kubwa sana kule Bududa. Watu kutoka Iburwa walikwenda pale sokoni kununua na kuuza bidhaa zao. Siku moja msichana mmoja mwenye umri wa miaka kama sita hivi jina lake Nabarwa alipotea njia na akafuatilia watu wanaokwenda Iburwa. Watu hao walienda naye hadi kwao. Msichana huyo alikua na kuwa mtu mzima. Baadaye, alipata mwanamume na akaolewa. Yeye alianza kuzaa watoto. Watoto wake wakawa wanatahiriwa. Inasemekana siku moja watu wa Bududa walipokuwa njiani wanakwenda Kenya kupitia Iburwa walimwona mwanamke aliyefanana sana na Nabarwa. Mmoja wao akauliza wenzake kwamba ni nani huyu anayefanana sana na Nabarwa? Yeye mwenyewe aliposikia hivyo alikiri kwamba ni yeye. Alisalimiana nao kisha akawapeleka nyumbani na kuwaandalia chakula. Walipokuwa huko, Nabarwa aliwaelezea desturi za huko na jinsi watoto wake walivyotahiriwa. Inasemekana watu hao kutoka Bududa walipendezwa sana na maelezo ya Nabarwa kuhusu tohara na wao pia wakaamua kuanzisha desturi hiyo ya tohara. Na kwamba kuanzia hapo Wamasaaba wakawa wanatahiri watoto wao wa kiume. Mifano hii mbalimbali ni muhimu sana na imewawekea Wamasaaba msingi wa fasihi simulizi. Vilevile imetupa mwanga wa kuelewa nafasi na umuhimu wa hadithi katika jamii ya Wamasaaba.

## 4.0 Nadharia Inayoongoza Utafiti huu

Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Ethnografia na Utendaji. Mwasisi wa nadharia hii ni Magoulick (1958) ambaye alisema kuwa Nadharia ya Ethnografia na Utendaji ilitokana na kutathmini na kuelewa watu na ubunifu wao katika hali halisi ya kimaisha. Nadharia hii huwa inazingatia usimulizi na maana zilizopo na jinsi zinavyopokelewa na jamii. Nadharia hii huwa inalenga usanii wa jamii. Aidha, nadharia hii huwa inahusisha hadithi na tukio fulani na kumthamini mwanasanaa husika. Nadharia hii inasisitiza sana mwanasanaa mwenyewe, hali ya utendaji, mandhari, hadhira na jamii nzima kwa jumla. Kwa hiyo, nadharia hii ilituwezesha kufafanua kwa nini masimulizi ya kinathari yamepungua katika jamii ya Wamasaaba wa Bududa na hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuimarisha utamaduni wa kusimulia hadithi.

## 5.0 Tafiti kuhusu Masimulizi ya Kihadithi

Ni vema katika sehemu hii tupitie maandiko kadhaa ili tuweze kuuelewa uga wa hadithi na kuweza kuona mchango wa utafiti huu wa sasa. Lakareber (2004) ameshughulikia mchango wa masimulizi ya kinathari katika kuboresha maadili na tabia za wasichana miongoni mwa Wacholi nchini Uganda. Utafiti wake umebaini kuwa hadithi nyingi miongoni mwa Wacholi zinalenga watoto wa kike kwa sababu yafaa msichana kushika tabia nzuri kwa sababu anapoolewa huwa anajiunga na jamii nyingine tofauti. Hivyo ingekuwa jambo la aibu kwa jamii iliyomlea kama msichana aliyeolewa angepatikana na tabia mbaya. Hivyo hadithi hizo zililenga kukuza maadili kwa wasichana, kuhimiza kufanya kazi kwa bidii, usafi, tabia nzuri, upole, utangamano, kupenda utamaduni, ubunifu na uwerevu. Maelezo haya yanaonyesha kwamba usimulizi wa hadithi ni

muhimu sana katika malezi ya watoto. Hivyo basi, kuna sababu maalumu kwa utafiti huu kutaka usimulizi wa hadithi uimarishwe katika jamii husika.

Kembabazi (2000) alitafiti masimulizi ya kinathari miongoni mwa jamii ya Wakiga inayopatikana magharibi mwa nchi ya Uganda. Utafiti wake unaonesha kuwa kwa kawaida hadithi zilipendwa na wanajamii hao kwani mbali na kupata burudani zinasaidia kuwaweka watu pamoja, hupunguza uchovu baada ya kazi za siku nzima na hujenga talanta miongoni mwa wasimulizi. Hadithi pia husaidia kupitisha muda ili kuwafanya watoto wasilale kabla ya kula chakula cha usiku. Kwani kwa kawaida watoto hulala mapema. Makala yetu inaona kwamba jamii inayokosa utamaduni wa kusimulia hadithi huwa na upungufu fulani. Jambo hili linaonyesha kwamba jamii ya Wamasaaba kama jamii zingine kote ulimwenguni inastahili kuendeleza utamaduni wa kusimulia hadithi. Na hapa tunaona sababu iliyomfanya mtafiti kuendeleza utafiti huu.

Kwa upande wake, Mushengyezi (1999) ameshughulikia visasili na mighani katika jamii ya Wanyankole nchini Uganda. Mushengyezi anasema kwamba mighani, yaani maelezo ya kihistoria kuhusu watu na matukio yanayokumbukwa katika jamii, ni muhimu sana kwa jamii. Madhumuni ya mighani ni kuwaelezea na kuheshimu mashujaa ambao wamewekea jamii misingi ya kihistoria. Kwa kawaida mighani huwa inazungumzia michango ya mashujaa katika jamii zao na jinsi mashujaa hao walivyokomboa jamii zao. Hapa, inabainika wazi kuwa masimulizi ya kihadithi ni muhimu sana na yanastahili kulindwa ili yasitoweke katika jamii zetu, jambo ambalo mtafiti anajaribu kulitekeleza katika utafiti huu.

Kwa mujibu wa Bastian (1999), utamaduni wa kusimulia hadithi hutofautiana kote ulimwenguni, ingawa kuna mambo mengi yanayofanana. Bastian alikusanya taarifa kuhusu desturi za kusimulia hadithi katika nchi mbalimbali. Katika utafiti wake aligundua kuwa watu wengi siku hizi wameanza kugundua furaha ya kusimulia hadithi, baada ya tamaduni zao kupoteza mambo mengi ya kusimulia hadithi na ambayo siyo rahisi wao kuyapata mambo hayo muhimu ya karne nyingi zilizopita. Jambo moja linalostahili kuzingatiwa ni kwamba katika tamaduni nyingi za kale, usimulizi wa hadithi huhusishwa na uimbaji wa nyimbo au muziki hasa katika tamaduni za Wabadiki wa Mashariki ya Kati. Hadithi hizo zinaweza kuimbwa zikiambatana na upigaji wa ala za muziki. Kulingana na maelezo haya, inabainika wazi kuwa masimulizi ya kihadithi huwa yanahifadhi mambo muhimu yanayohusu jamii zetu na yanastahili kuendelezwa ili tusipoteze misingi ya utamaduni wetu. Hili ni jambo ambalo mtafiti anajaribu kulifanya katika makala hii.

Lihamba (1980) ameangalia sanaa za maonyesho nchini Tanzania na anasema kwamba usimulizi wa hadithi ni mojawapo ya tanzu za sanaa za maonyesho. Yeye anasema kwamba sanaa za maonyesho zinahitaji maandalizi maalumu na kwa kawaida mwanasanaa huwa anateua dhana fulani na kuzipanga kwa njia inayoweza kugusa hisia

za hadhira na kutoa picha halisi ya kile anachotaka kuwasilisha. Lihamba anasema kuwa kama ilivyo kwa tanzu zingine za sanaa za maonyesho, msimulizi wa hadithi hutekeleza kazi yake kwa njia mbili. Kwanza, inambidi akusanye taarifa za mambo anayoyaona na kuyasikia katika maisha yake ya kawaida na kufanya utafiti huku akitafuta majibu kwa maswali tofauti kuhusu utendaji katika sanaa za maonyesho. Mwanasanaa huwa anakusanya taarifa hizo zote na kuzihifadhi mpaka anapozihitaji. Pili, baada ya kukusanya taarifa ni utendaji halisi mbele ya hadhira. Lihamba anasema kwamba hapa ndipo mwanasanaa hutumia ujuzi wake kikamilifu kama vile matumizi ya mwili wake, sauti, matendo na kuonyesha usanii wake kwa jumla. Maelezo ya mtaalamu huyu yanaonyesha kwamba utendaji halisi hufanya masimulizi ya kihadithi kuwa utanzu maalumu wa sanaa ya maonyesho. Kwa hiyo, utanzu huu unastahili kuchunguzwa na kuendelezwa kama ilivyo kwa tanzu zingine, jambo ambalo makala hii inajaribu kulitekeleza katika utafiti huu.

Kwa mujibu wa Agatucci (2003), kiutamaduni Waafrika wana hadithi nyingi zinazozungumzia watu mashuhuri katika jamii. Maandishi ya kwanza yanapatikana Afrika lakini Waafrika wengi kama ilivyokuwa siku za kale ni watu wanaoheshimu masimulizi ya kinathari kuliko maandishi. Hadithi za Kiafrika hutungwa na kuendelezwa kwa njia ya mdomo. Kazi hizi za Kiafrika ni nyingi na zinatofautiana. Kazi hizo zinatokana na tamaduni za Kiafrika na zinabakia hai na zimeendelea kustawi mpaka leo. Kulingana na taarifa hii, lengo hili linasisitizwa na kutekelezwa katika masimulizi ya kale. Katika masimulizi hayo, tabia mbaya ambazo hazifai katika jamii huwa zinadhihirishwa. Kulingana na taarifa hii, Waswahili katika pwani ya Kenya na Tanzania wana lundo la hadithi zenye vipengele vya dini ya Kiislamu. Aidha, Waswahili hao wana hadithi zinazozungumzia hila za Sungura, ujinga wa Fisi, majini, mashujaa, wakarimu na wenye busara. Hali kadhalika, miongoni mwa Wahaya kule Tanzania vijana hupata historia ya familia zao kupitia masimulizi ya kinathari. Jambo hili linafanya vijana hao kujitambulisha na watu wenye sifa fulani na kujaribu iwezekanavyo kuiga tabia hizo. Ni jambo la kusitikisha kuona masimulizi ya kihadithi yanaendelezwa katika jamii nyingi huku yakiwa yanapuuzwa na Wamasaaba. Jambo hili lilipelekea mtafiti kufanya uchunguzi huu ili kuziba pengo hili.

Vilevile, Roberts (1995)[1] anasema kwamba fasihi simulizi imeanza kutoweka kwa kasi katika jamii za Kiafrika. Yeye anasema kuwa vijana wamechukuliwa sana na redio pamoja na runinga na hawana wakati wa kukaa chini na kusikiliza hadithi zinazosimuliwa na wazazi wao. Roberts anaendelea kusema kwamba kupungua kwa usimulizi wa hadithi kumepelekea tabia za vijana kuwa mbaya. Kwa bahati mbaya, mtaalamu huyu hajasema ni hatua gani ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuimarisha na kuendeleza utamaduni wa kusimulia hadithi katika jamii za Kiafrika. Na jambo hili

---

[1] Taz. http://www.cgpublisher.com/proposals/124/index-html, ulioangaliwa tarehe 17/05/2009.

limeacha mwanya ambao mtafiti ameuziba kwa kushughulikia usimulizi wa hadithi katika jamii ya Wamasaaba wa Bududa.

Kwa mujibu wa Mutembei (2013), fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo kuwapo kwake hutegemea sana masimulizi ya mdomo. Fasihi hii ndiyo kongwe zaidi duniani, na ndiyo mzazi wa fasihi andishi. Jamii zote zenye maandishi zilikuwa, na bado nyingine zinaendeleza usimulizi. Kupitia katika fasihi hii, wanajamii husimuliana matukio, huelimishana, huonyana na kupeana taarifa za makuzi na malezi kwa njia ya kisanaa na ubunifu bila ya kutumia maandishi. "Njia ya kisanaa na ubunifu" ndiyo maneno ya msingi ambayo huyafanya masimulizi haya kuwa ya kifasihi. Kwa hiyo, si kila masimulizi ni fasihi, ila tu yale yatumiayo njia ya kisanaa na ubunifu mkubwa. Katika miaka ya hivi karibuni utolewaji wa fasihi hii hasa nchini Tanzania umekumbwa na mabadiliko makubwa. Mabadiliko hayo ni matokeo ya kukua kwa teknolojia na matumizi ya vyombo vya kielektroniki. Kutoka katika hali ya kuonana wakiwa pamoja, msimuliaji na wasimuliwaji, sasa fasihi hii imeingia katika kuwasilishwa kupitia katika televisheni au redio. Imeweza kuwekwa katika kanda, santuri na video ili wale ambao hawakuwapo wakati wa usimuliaji waendelee kuisikia au kuona masimulizi husika, muda mwingine.

Kwa mujibu wa Mrikaria (2007), fasihi simulizi ndiyo fasihi ya awali. Aina hii ya fasihi imeanza wakati binadamu alipoanza kutumia lugha kama moja ya chombo cha mawasiliano. Kuanzia hapo ndipo mwanadamu alipoanza kuimba, kutumia methali, vitendawili, nahau na kadhalika. Kuwapo kwa maendeleo endelevu, kutokea kwa mapinduzi ya viwanda na baadaye kuingia kwa teknolojia mpya yalisababisha mabadiliko katika fani za fasihi simulizi. Mabadiliko haya yaliigawa fasihi simulizi katika fasihi simulizi ya zamani na fasihi simulizi ya kisasa au fasihi simulizi teknolojia mpya. Mrikaria (2007) anaeleza kuwa fasihi simulizi ya zamani ililenga zaidi katika kurithishana mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi kimoja (babu, bibi na wengineo wa umri wao) hadi kingine (watoto na wajuku zao). Anasema kuwa fasihi hii ilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia nyimbo, hadithi, ngoma, mashairi, na hata michezo ya ujasiri na majigambo. Maelezo haya ya Mrikaria yanaonyesha jinsi usimulizi wa kihadithi ulivyo muhimu na kuzua maswali kwa nini watu wa Bududa hawajachukua hatua za kuimarisha utamaduni huo wa kusimulia hadithi.

## 6.0 Sababu za Kupungua kwa Hadithi na Namna ya Kuziendeleza

Hapa tunafanya uchambuzi wa data kutoka njia mbalimbali ambazo tulitumia kukusanyia data, yaani mahojiano, hojaji na uchunguzi ushiriki tulioufanya kwa kuzingatia maswali yetu ya utafiti. Matokeo hayo ya data kulingana na utafiti wetu tunayawasilisha kwa kutumia majedwali. Tunaanza kuonesha sababu za kupungua masimulizi ya hadithi kisha tunabainisha namna ya kuendeleza masimulizi hayo katika jamii hiyo, baada ya hapo mjadala kuhusiana na data hizo unafuata.

### 6.1 Sababu za Kupungua kwa Masimulizi ya Kihadithi katika Jamii ya Wamasaaba

Jedwali lifuatalo linawasilisha sababu za kupungua kwa masimulizi ya kihadithi katika jamii ya Wamasaaba:

**Jedwali 1: Sababu za Kupungua kwa Hadithi**

| Hoja | Wanaokubali | % | Wasiokubali | % | Wasiojua jibu | % | Wasiokuwa na uhakika | % | Jumla ya majibu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Utendaji kutekelezwa kifamilia | 88 | 73.3 | 25 | 20.8 | 07 | 5.8 | 00 | 00 | 120 |
| Kwa kawaida hakuna matumizi ya ala za muziki | 92 | 76.7 | 22 | 18.3 | 05 | 4.2 | 01 | 0.8 | 120 |
| Hakuna matumizi ya maleba kwa kiwango kikubwa | 86 | 71.7 | 30 | 25 | 04 | 3.3 | 00 | 00 | 120 |
| Masimulizi hayo huzungumzia mambo ya kale | 95 | 79.2 | 25 | 20.8 | 00 | 00 | 00 | 00 | 120 |
| Hakuna maandalizi maalumu | 93 | 77.5 | 26 | 21.7 | 01 | 0.8 | 00 | 00 | 120 |
| Hadhira lengwa ni watoto | 90 | 75 | 17 | 14.2 | 13 | 10.8 | 00 | 00 | 120 |
| Hakuna kula na kunywa pombe ya bure | 94 | 78.3 | 21 | 17.5 | 05 | 4.2 | 00 | 00 | 120 |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2012)

Mtafiti alitafuta mapungufu ya masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba kwa sababu anafikiria kwamba mapungufu hayo ndiyo yamesababisha utamaduni wa kusimulia hadithi kutoweka katika jamii ya Wamasaaba. Na baada ya shughuli ya kuchanganua data kukamilika, matokeo yalidhihirisha mambo yafuatayo: Majibu themanini na manane (88) yakiwakilisha asilimia sabini na tatu nukta tatu (73.3%) yanaonyesha kwamba utendaji wa masimulizi ya kinathari huwa wa kifamilia na kwa kawaida hutekelezwa familia husika ikiwa ndani ya nyumba yao. Wahojiwa wote ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walikubaliana na hoja hiyo. Mhojiwa mmoja kwa jina Nasaka alimwambia mtafiti kuwa katika jamii ya Wamasaaba, utendaji wa masimulizi ya kinathari ni wa kifamilia. Alisema kuwa hadhira huwa ni watoto na watu huwa hawakusanyiki kutoka familia mbalimbali. Majibu ishirini na matano (25) yakiwakilisha asilimia ishirini nukta nane (20.8%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali jambo hilo. Na majibu saba (07) yakiwakilisha asilimia tano nukta nane (5.8%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi.

Majibu tisini na mawili (92) yakiwakilisha asilimia sabini na sita nukta saba (76.7%) yanaonyesha kwamba utendaji wa masimulizi ya kinathari miongoni mwa Wamasaaba kwa kawaida hauhusishi ala za muziki. Wahojiwa wote ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kwamba katika utendaji wa masimulizi ya kinathari hakuna matumizi ya ala za muziki kwa kiwango kikubwa. Mhojiwa mmoja kwa jina Khawanga alimwambia mtafiti kuwa mara nyingi wasimulizi wa hadithi hawatumii ala za muziki katika utendaji wao. Majibu ishirini na mawili (22) yakiwakilisha asilimia kumi na nane

nukta tatu (18.3%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali jambo hilo. Majibu matano (05) yakiwakilisha asilimia nne nukta mbili (4.2%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi. Na jibu moja (01) likiwakilisha asilimia sifuri nukta nane (0.8%) linaonyesha kwamba mhojiwa husika hakuwa na uhakika kuhusu jibu sahihi.

Majibu themanini na sita (86) yakiwakilisha asilimia sabini na moja nukta saba (71.7%) yanaonyesha kwamba katika utendaji wa masimulizi ya kinathari, kwa kawaida wahusika huwa hawatumii maleba. Wahojiwa wote ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walikana jambo hilo. Mhojiwa mmoja kwa jina Shibuta alisisitiza kuwa katika utendaji wa masimulizi ya kinathari, hakuna kabisa matumizi ya maleba. Majibu thelathini (30) yakiwakilisha asilimia ishirini na tano (25%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubaliana na hoja. Na majibu manne (04) yakiwakilisha asilimia tatu nukta tatu (3.3%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi. Majibu tisini na mawili (92) yakiwakilisha asilimia sabini na sita nukta saba (76.7%) yanaonyesha kwamba ujumbe katika masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba huwa unaashiria matukio yaliyopita. Wahojiwa wote walikubali kwamba masimulizi yote ya kinathari ya Wamasaaba huwa yakiashiria matukio yaliyopita. Mhojiwa mmoja kwa jina Kuloba alisema kuwa hajawahi kusikia hadithi yoyote katika jamii yao ambayo inaeleza matukio yaliyopo au yajayo. Alisisitiza kuwa matukio yote yanayoelezwa katika masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba huwa yanaeleza matukio ya karne zilizopita. Majibu ishirini na matano (25) yakiwakilisha asilimia ishirini nukta nane (20.8%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubaliana na hoja iliyotolewa. Na majibu matatu (03) yakiwakilisha asilimia mbili nukta tano (2.5%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi.

Majibu tisini na matatu (93) yakiwakilisha asilimia sabini na saba nukta tano (77.5%) yanaonyesha kwamba katika utendaji wa masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba hakuna maandalizi ya kina. Wahojiwa wote ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kuwa hakuna maandalizi ya kina katika utendaji wa masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba. Mhojiwa mmoja kwa jina Kibeti alimwambia mtafiti kuwa katika utendaji wa masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba, watu huwa hawachukui muda kufanya maandalizi kama ilivyo kwa matukio mengine. Majibu ishirini na sita (26) yakiwakilisha asilimia ishirini na moja nukta saba (21.7%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja. Na jibu moja (01) likiwakilisha asilimia sifuri nukta nane (0.8%) linaonyesha kwamba mhojiwa husika hakujua jibu sahihi.

Majibu tisini (90) yakiwakilisha asilimia sabini na tano (75%) yanaonyesha kwamba katika masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba, hadhira lengwa huwa ni watoto. Wahojiwa wote ambao walisailiwa moja kwa moja walisema kwamba hadhira katika masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba ni watoto wadogo. Mhojiwa mmoja kwa jina Wakwale alimwambia mtafiti kuwa masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba huwa

yakilenga watoto wadogo wala siyo watu wazima. Majibu kumi na saba (17) yakiwakilisha asilimia kumi na nne nukta mbili (14.2%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja iliyotolewa. Na majibu kumi na matatu (13) yakiwakilisha asilimia kumi nukta nane (10.8%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu ambalo lilikuwa sahihi miongoni mwa yale ambayo yalikuwa yametolewa.

Majibu tisini na manne (94) yakiwakilisha asilimia sabini na nane nukta tatu (78.3%) yanaonyesha kwamba katika utendaji wa masimulizi ya kinathari ya Wamasaaba hakuna kula chakula na kunywa pombe ya bure kama ilivyo na utendaji wa sherehe za tohara. Wahojiwa wote ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kuwa katika utendaji wa masimulizi ya kinathari, hakuna kula chakula na kunywa pombe ya bure. Mhojiwa mmoja kwa jina Watsyeli alimwambia mtafiti kuwa jambo la kutokula chakula na kunywa pombe ya bure ndiko kumefanya masimulizi ya kinathari kupungua. Majibu ishirini na moja (21) yakiwakilisha asilimia kumi na saba nukta tano (17.5%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja iliyotolewa. Na majibu matano (05) yakiwakilisha asilimia nne nukta mbili (4.2%) yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu ambalo lilikuwa sahihi miongoni mwa yale ambayo yalikuwa yametolewa.

### 6.2 Namna ya Kuimarisha Utamaduni wa Kusimulia Hadithi katika Jamii ya Wamasaaba

Kwa mujibu wa utafiti wetu hoja mbalimbali zimetolewa ili kuimarisha usimulizi wa hadithi katika jamii ya Wamasaaba. Jedwali hapa chini linawasilisha hoja hizo:

**Jedwali 2: Hatua za Kufufua Utamaduni wa Kusimulia Hadithi katika Jamii ya Wamasaaba**

| Hoja | Wanakubali | % | Hawakubali | % | Hawajui | % | Hawana uhakika | % | Jumla ya majibu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga majumba ambamo hadithi husimuliwa | 103 | 85.8 | 12 | 10 | 05 | 4.2 | 00 | 00 | 120 |
| Kuanzisha kamati za kushughulika na mambo ya kusimulia hadithi | 93 | 77.5 | 21 | 17.5 | 06 | 05 | 00 | 00 | 120 |
| Wasimulizi bora wazawadiwe | 100 | 83.3 | 17 | 14.2 | 03 | 2.5 | 00 | 00 | 120 |
| Usimulizi wa hadithi kuwa katika mtaala wa elimu | 95 | 79.2 | 20 | 16.7 | 04 | 3.3 | 01 | 0.8 | 120 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usimulizi wa hadithi kuwa mojawapo ya masomo katika vyuo vikuu | 91 | 75.8 | 18 | 15 | 11 | 9.2 | 00 | 00 | 120 |
| Wasimulizi bora waajiriwe na serikali | 89 | 74.2 | 19 | 15.8 | 11 | 9.2 | 01 | 0.8 | 120 |
| Kuelimisha jumuiya kwa kutumia vituo vya matangazo | 85 | 70.8 | 29 | 24.2 | 04 | 3.3 | 02 | 1.7 | 120 |
| Usimulizi wa hadithi kuwa mojawapo ya masharti kwa wale wanaotaka kuingia katika siasa | 77 | 64.2 | 21 | 17.5 | 22 | 18.3 | 00 | 00 | 120 |
| Majina ya wasimulizi bora kuchapishwa | 87 | 72.5 | 16 | 13.3 | 16 | 13.3 | 01 | 0.8 | 120 |
| Usimulizi wa hadithi upelekwe nje ya familia | 94 | 78.3 | 10 | 8.3 | 15 | 12.5 | 01 | 0.8 | 120 |
| Wasimulizi wa hadithi wafadhiliwe na serikali | 92 | 76.7 | 23 | 19.2 | 03 | 2.5 | 02 | 1.7 | 120 |
| Watu wasioshiriki katika usimulizi wa hadithi watozwe kodi | 73 | 60.8 | 25 | 20.8 | 18 | 15 | 04 | 3.3 | 120 |

Chanzo: Data za uwandani (2012)

Kulingana na jedwali hili, majibu mia moja na thelathini (103) yakiwakilisha asilimia themanini na tano nukta nane (85.8%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba usimulizi wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba unaweza kuimarishwa kwa kujenga majumba ambamo shughuli za kusimulia hadithi zinaweza kuendelezwa. Wahojiwa ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kwamba kuwapo kwa majumba hayo kunaweza kuhamasisha watu kushiriki katika usimulizi wa hadithi. Mhojiwa mmoja kwa jina Walimbwa alisisitiza kuwa majengo kama hayo yakijengwa, watu wanaweza kuona umuhimu wa kusimulia hadithi. Hata hivyo, majibu kumi na mawili (12) yakiwakilisha asilimia kumi (10%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubaliana na hoja. Na majibu matano (05) yakiwakilisha asilimia nne nukta mbili (4.2%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi.

Majibu tisini na matatu (93) yakiwakilisha asilimia sabini na saba nukta tano (77.5%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba ili kuimarisha usimulizi wa hadithi yafaa kamati maalumu zinazowajibika na maandalizi ya usimulizi wa hadithi ziundwe. Wahojiwa wote ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kuwa kamati za kuandaa mashindano katika usimulizi wa hadithi zikibuniwa zinaweza kufanya usimulizi wa hadithi kuimarika. Mhojiwa mmoja kwa jina Walimbwa alisema kwamba jambo hilo linaweza kusababisha usimulizi wa hadithi kuimarishwa kwa sababu washiriki watajaribu iwezekanavyo kuona kwamba wanaibuka washindi. Hata hivyo, majibu ishirini na moja (21) yakiwakilisha asilimia kumi na saba nukta tano (17.5%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja. Na majibu sita (06) yakiwakilisha asilimia tano (05%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi.

Majibu mia moja (100) yakiwakilisha asilimia themanini na tatu nukta tatu (83.3%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba ili kuimarisha usimulizi wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba, kuna mahitaji ya kuhamasisha watu kushiriki katika mashindano ya kusimulia hadithi kwa kuwazawadia wasimulizi bora. Wahojiwa wote ambao walisailiwa moja kwa moja walikubali hoja hiyo. Mhojiwa mmoja kwa jina Mulokwa alimwambia mtafiti kuwa ili kufanya usimulizi wa hadithi uimarike katika jamii ya Wamasaaba wakazi wanasitahili kuhamasishwa kushiriki katika mashindano ya kusimulia hadithi. Majibu kumi na saba (17) yakiwakilisha asilimia kumi na nne nukta mbili (14.2%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja. Na majibu matatu (03) yakiwakilisha asilimia mbili nukta tano (2.5%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi. Majibu tisini na matano (95) yakiwakilisha asilimia sabini na tisa nukta mbili (79.2%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba ili kuimarisha usimulizi wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba kuna haja ya kuingiza usimulizi wa hadithi katika mtaala wa elimu ili wanafunzi washughulikie sanaa hii kama somo lolote jingine. Wahojiwa ambao Walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kwamba kuweka usimulizi wa hadithi kwenye mtaala wa elimu kunaweza kusababisha wanafunzi kufanya jitihada za kusimulia hadithi wakihofia kuanguka mtihani.

Mwalimu mstaafu kwa jina Kusolo alisema kuwa usimulizi wa hadithi ukiwekwa kwenye mtaala wa elimu utaendeleza sanaa hii kwa sababu wanafunzi wote watajitahidi kufaulu mtihani. Hata hivyo, majibu ishirini (20) yakiwakilisha asilimia kumi na sita nukta saba (16.7%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja. Majibu manne yakiwakilisha asilimia tatu nukta tatu (3.3%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi. Na jibu moja (01) likiwakilisha asilimia sifuri nukta nane (0.8%) ya majibu yote linaonyesha kwamba mhojiwa husika hakuona jibu sahihi miongoni mwa yale ambayo yalikuwa yamependekezwa.

Majibu tisini na moja (91) yakiwakilisha asilimia sabini na tano nukta nane (75.8%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba ili kuimarisha usimulizi wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba, yafaa jambo lenyewe lifanywe kuwa somo maalumu katika Vyuo Vikuu na watu wapewe shahada katika usimulizi wa hadithi. Wahojiwa ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kwamba jambo hili likitekelezwa linaweza kuchangia uimarishaji wa utamaduni wa kusimulia hadithi katika jamii ya Wamasaaba. Mwalimu Kusolo alisema kuwa Vyuo Vikuu vikianza kutoa shahada katika usimulizi wa hadithi, wanafunzi wataendeleza sanaa hii wakitaka kufaulu mtihani. Hata hivyo, majibu kumi na manane (18) yakiwakilisha asilimia kumi na tano (15%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja. Na majibu kumi na moja (11) yakiwakilisha asilimia tisa nukta mbili (9.2%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi.

Majibu themanini na tisa (89) yakiwakilisha asilimia sabini na nne nukta mbili (74.2%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba ili kuimarisha usimulizi wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba yafaa wasimulizi bora waajiriwe na serikali kisha walipwe mishahara kama wafanyakazi wengine katika sekta ya umma. Wahojiwa ambao walikutana na mtafiti ana kwa ana walisema kwamba wasimulizi bora wanaweza kuajiriwa kama wasimamizi wa vituo ambako hadithi husimuliwa katika jamii, walimu katika shule za msingi na za sekondari na hata katika Vyuo Vikuu. Mhojiwa mmoja kwa jina Wambette alimwambia mtafiti kuwa wasimulizi mahiri wakiajiriwa shuleni kama walimu, wataendeleza sanaa hii katika jamii ya Wamasaaba. Hata hivyo, majibu kumi na tisa (19) yakiwakilisha asilimia kumi na tano nukta nane (15.8%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakukubali hoja. Majibu kumi na moja (11) yakiwakilisha asilimia tisa nukta mbili (9.2%) ya majibu yote yanaonyesha kwamba wahojiwa husika hawakujua jibu sahihi. Na jibu moja (01) tu likiwakilisha asilimia sifuri nukta nane (0.8%) ya majibu yote linaonyesha kwamba mhojiwa husika hakuwa na uhakika kuhusu jibu sahihi.

### 6.3 Mjadala wa Data za Utafiti

Kwa kuangalia data za utafiti wetu imebainika wazi kuwa usimulizi wa hadithi katika jamii ya Wamasaaba wa Bududa umepungua kutokana na sababu mbalimbali. Idadi kubwa ya wahojiwa wametaja sababu kadhaa zinazofanya kupungua kwa usimulizi wa hadithi katika jamii hii. Miongoni mwa sababu hizo ni kukosekana kwa matumizi ya ala za muziki katika utendaji wa hadithi. Ingawa kutoka zamani ala za muziki zilikuwa hazitumiki katika masimulizi ya hadithi lakini kutokana na maendeleo ya jamii hivi leo jambo hili halina budi kuingizwa katika usimulizi wa kihadithi. Na hii inatokana na ukweli kwamba muziki ni moja ya fani muhimu katika jamii hivyo haina budi kuingizwa katika utendaji wa hata tanzu ambazo hapo zamani zilikuwa hazitumii muziki, kama vile hadithi. Hali kadhalika, utafiti umegundua kuwa utendaji kuendelea kufanywa katika ngazi ya kifamilia na kukosekana kwa matumizi ya maleba miongoni mwa fanani kumechangia kudumaza hadithi katika jamii. Ni kweli kwamba hata zamani

usimulizi wa kihadithi ulikuwa ukitekelezwa kifamilia na bila kutumia maleba lakini kutokana na maendeleo ya ulimwengu hali hii inapaswa kufanyiwa marekebisho. Hii ni pamoja na kupeleka usimulizi wa kihadithi nje ya familia na fanani kutumia maleba ili kuimarisha utanzu husika kisanaa. Sababu nyingine ni kwa masimulizi hayo kuendelea kuzungumzia mambo ya kale na ambayo labda yamepitwa na wakati. Kwa hiyo, jamii katika utunzi wa hadithi zake hazina budi kuingiza mambo ya hivi karibuni ili kufanya hadhira ipate picha kamili. Sababu nyingine ni kuwapo kwa hadhira ya watoto wadogo. Utamaduni uliozoeleka ni kwamba hadhira ya hadithi ni watoto wadogo, hivyo inashauriwa kuwa katika ulimwengu wa leo usimulizi wa kihadithi uhusishe hadhira ya watu wazima. Katika kufanikisha jambo hili majumba maalum ya kusimulia hadithi yajengwe ambamo hadithi zitasimuliwa. Kwa kufanya hivi kutaimarisha usimulizi wa hadithi na kuinua hali ya kiuchumi katika jamii husika. Hii ni kwa sababu pesa ambazo watu wanaoshiriki katika mashindano ya kusimulia hadithi hupewa wanaweza kuziwekeza katika biashara na hivyo kujiinua kiuchumi. Aidha, kodi zinazotozwa na serikali ya wilaya ya Bududa kwa watu wasioshiriki katika usimulizi wa kihadithi zinaweza kutumiwa kuanzisha miradi inayoleta maendeleo kwa wakazi na hivyo kuwainua kiuchumi.

Sababu nyingine ni kukosekana kwa kula na kunywa pombe ya bure watu wanaposimulia hadithi. Ni kweli kwamba familia hizi zina vyakula lakini utendaji wenyewe hauonekani kuwa sherehe maalum na hii ndiyo sababu upungufu unaojadiliwa umetokea. Kwa kawaida, mambo ya kijamii huwa na uzito kama kuna kula na kunywa bila kulipia na kuhusisha jamii nzima. Kwa hiyo, usimulizi wa kihadithi ukipelekwa nje ya familia na kuhusisha watu wazima kisha vyakula na vinywaji visivyo vya kulipia vikatolewa, basi bila shaka usimulizi wa kihadithi utapata nguvu katika jamii husika. Ili kuondoa tatizo hili serikali ya Wilaya ya Bududa inaweza kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli hiyo. Kulingana na data tulizowasilisha ni idadi ndogo sana ya wahojiwa ambayo ilipinga au haikujua majibu sahihi.

Aidha, data za utafiti wetu zimebaini kuwa usimulizi wa hadithi katika jamii ya Wamasaaba unaweza kuimarishwa na kushamiri zaidi. Miongoni mwa hatua za kuchukua kwa mujibu wa utafiti wetu, kama tulivyokwishasema hapo awali, ni kujenga majumba ambamo hadithi zinaweza kusimuliwa na kuanzisha kamati maalumu ya kushughulika na mambo ya kusimulia hadithi. Kamati hii inaweza kuundwa na serikali ya Wilaya ya Bududa ili kuendeleza shughuli hii kama inavyofanya katika kuendeleza kandanda na michezo mingineyo. Hatua nyingine za kuchukuliwa ni kuwazawadia wasimulizi bora wa hadithi, na usimulizi wa hadithi ufanywe kuwa mojawapo ya kozi katika Vyuo Vikuu.

Vilevile, wasimulizi bora waajiriwe na serikali ya Wilaya hiyo kama walimu wa kufundisha somo la kusimulia hadithi katika shule za msingi na zile za sekondari. Hatua nyingine ni kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa kusimulia hadithi kwa kutumia

vyombo vya habari na vituo vya matangazo. Aidha, usimulizi wa hadithi unapaswa kufanywa kuwa mojawapo ya masharti kwa wale wanaotaka kuingia katika siasa. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa usimulizi wa hadithi unaimarishwa. Kwa hiyo, tukitumia wanasiasa katika ngazi mbalimbali kuanzia za serikali ya mitaa hadi bungeni, tunaweza kutimiza lengo letu. Kwa sababu watu wengi huwa na hisia za kutaka kujiunga na siasa, watu hawa wakilazimishwa kisheria kusimulia hadithi, jamii ya Wamasaaba itanufaika sana kwa sababu utamaduni wao utaimarishwa.

Na mwishowe, sisi wanafasihi pia tutanufaika kwa sababu tutakuwa na mambo mengi ya kuzungumzia katika nyanja yetu. Hatua nyingine za kuchukua ni majina ya wasimulizi bora yachapishwe kwenye mtandao wa intaneti na usimulizi wa hadithi upelekwe nje ya familia. Vilevile, wasimulizi wa hadithi wafadhiliwe kifedha na serikali ya Wilaya ya Bududa kila wanapokwenda kushiriki katika usimulizi wa kihadithi. Serikali iwe na bajeti kwa shughuli hiyo ili iweze kutoa nauli, vinywaji na vyakula wakati watu wanaposimulia hadithi. Kodi hii inaweza kuitwa kodi ya kusimulia hadithi. Watu watozwe kodi hii katika hadithi pekee kwa sababu tanzu zingine za fasihi zimekwishapata maendeleo. Kodi hii itawafanya watu kushiriki katika usimulizi wa hadithi. Data za utafiti wetu kama inavyoonekana katika jedwali ni idadi ndogo sana ya wahojiwa ambayo ilipinga au haikujua majibu sahihi au haikuwa na uhakika. Lakini idadi kubwa ya wahojiwa kama inavyobainishwa na asilimia mbalimbali kwenye data inaonyesha kwamba hizi ndizo hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ili usimulizi wa hadithi upate kuimarishwa katika jamii ya Wamasaaba wa Bududa. Kwa upande wake, mtafiti pia anakubaliana na hatua hizi. Ni kweli kwamba inaweza kuwa vigumu kutekeleza hatua hizi zote lakini baadhi yake zikitekelezwa tunaweza kuwa na matumaini kwamba usimulizi wa kihadithi utaimarishwa katika jamii husika.

## 7.0 Hitimisho

Makala hii imeonesha kwamba usimulizi wa hadithi ni muhimu sana katika jamii hususani katika uboreshaji wa mienendo ya vijana. Usimulizi wa hadithi ni njia mojawapo ya kuwapa vijana elimu. Mbali na kuwapa vijana elimu, usimulizi wa hadithi huchangamsha watu na kuwaondolea uchovu. Makala imebainisha mambo mbalimbali yanayosababisha kudorora kwa usimuliaji wa hadithi miongoni mwa Wamasaaba. Na kwa sababu hizi, jamii mbambali ikiwamo ya Wamasaaba wa Bududa zinastahili kuchukua hatua madhubuti ili kuimarisha utamaduni wa kusimulia hadithi.

## Marejeleo

Agatucci Cora (2003), *African Storytelling*, Central Oregon Community College.

Kembabazi, M. (2000). *The Entertainment Role of Folktales among the Bakiga* – a Dissertation (BA, Educ.), Kampala, Makerere University.

Lakareber, J. (2004). *The Role of FolkTales in Shaping Morals and Behaviour of Girls and Young Women among the Acoli* – A Dissertation (BA, Educ.), Kampala, Makerere University.

Lihamba, A. (1980). *'Tale – Telling as a Performing Art – A Comparative Study,'* Department of

Art, Music and Theatre, University of Dar es Salaam.
Mrikaria, S. (2007), Fasihi Simulizi, *Swahili Forum* 14: 197 -206
Mushengyezi, A. (1999). *Towards a Psychoanalytic Understanding of Folk Myths and Legends on Cultural Ideology in Akole*, A Dissertation (MA), Makerere University, Kampala.
Mutembei A. K (2013). *Hali na Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili katika Tanzania*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Nzita and Mbaga – Niwampa. (1998). *Peoples' and Cultures of Uganda*, Kampala, Fountain Publishers Ltd.

**Tovuti**

http://www.cgpublisher.com/proposals/124/index-html seen on 17/05/2009
http://www. timsheppard.co.uk/story/dir/traditions/African.html seen on 12/04/2009
http://www.wikipedia.org/wiki/.../Usimulizi_wa_Hadithi_Keny seen on 05/06/2014
http://www.tanzania-network.de/front_content.php?idart=71 seen on 07/06/2014
https://www.womensrights.informationactivism.org/.../kusim seen on 02/07/2014